

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 23 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka wa wanahisa wa Benki ya NMB utafanyika kwa njia ya mtandao kuanzia saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 2, 2023. Agenda itakuwa kama ifuatavyo:

- 23.1 MATANGAZO NA AKIDI
- 23.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 23.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 22 ULIOFANYIKA TAREHE 3 JUNI 2022
- 23.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 22 WA WANAHISA
- 23.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022
- 23.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022
- 23.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI
- 23.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI
- 23.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DISEMBA 2023
- 23.10 MENGINEYO

MAELEZO MUHIMU

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria Mkutano lazima wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (Depositoty receipt).
2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano binafsi kwa njia ya mtandao wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi wataohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki NMB Makao Makuu au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe Consolatha.Resto@nmbbank.co.tz kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 1 Juni 2023.
3. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria kikao watahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za uwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya Benki ya NMB (www.nmbbank.co.tz).
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 286 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 143.1 bilioni, kutokana na faida ya mwaka 2022.

Tarehe za kuzingatia:

Tarehe ya tangazo:	- 12 Mei 2023
Hisa kuuzwa pamoja na gawio :	- 12 Mei 2023
Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :	- 31 Mei 2023
Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:	- 1 Juni 2023
Daftari la wanahisa kufungwa:	- 5 Juni 2023
Malipo ya gawio kwa wanahisa: kuanzia tarehe	- 14 Juni 2023

Kwa agizo la Bodi.



Consolatha R. Moshia

Kaimu Katibu wa Kampuni

12 Mei 2022